N15/2/ABSWA/SP1/SWA/TZ0/XX/T

Diploma Programme
Programme du diplôme
Programa del Diploma

# Swahili B – Standard level – Paper 1
# Swahili B – Niveau moyen – Épreuve 1
# Swahili B – Nivel medio – Prueba 1

Monday 9 November 2015 (afternoon)
Lundi 9 novembre 2015 (après-midi)
Lunes 9 de noviembre de 2015 (tarde)

1 h 30 m

---

**Text booklet – Instructions to candidates**

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for paper 1.
- Answer the questions in the question and answer booklet provided.

**Livret de textes – Instructions destinées aux candidats**

- N’ouvrez pas ce livret avant d’y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l’épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

**Cuaderno de textos – Instrucciones para los alumnos**

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

8815 – 2319



© International Baccalaureate Organization 2015

International Baccalaureate
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

https://xtremepape.rs/

**Kifungu A**

# Juhudi zahitajika kuhifadhi mazingira



❶ Wiki iliyopita, mataifa mengi, ikiwemo Kenya yaliadhimisha siku ya mazingira duniani. Maadhimisho hayo hayakufanywa kwa shangwe nyingi kama inavyokuwa wakati wa maadhimisho mengine kama vile siku ya Ukimwi au Saratani, ambayo huendelea hata kwa wiki moja au mwezi mzima.

❷ Hii ni ishara kuwa masuala ya mazingira hayachukuliwi kwa uzito unaostahili. Kadiri na jinsi miaka inavyosonga ndivyo hali ya mazingira inavyozidi kuzorota katika mataifa yote ulimwenguni. Lakini binadamu tumejifanya hamnazo na kufumbia macho athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira.

❸ Athari hizo zinajumuisha njaa, magonjwa na umaskini. Hali mbaya ya hewa huathiri vibaya uzalishaji wa chakula na hiyo ndiyo sababu tunaona sehemu nyingi ulimwenguni zikikumbwa na janga la njaa. Hapa Kenya, matukio mbalimbali kama vile ukame na mafuriko yanayotokea wakati ambao hayatarajiwi ni kati ya athari za uharibifu wa mazingira. Licha ya kuwa taarifa nyingi za habari huonyesha tu mataifa ya Afrika yakikabiliwa na majanga kama haya, kuna ripoti iliyotolewa majuzi inayoonyesha hali hiyo hushuhudiwa hata Amerika ambapo iliripotiwa kuna hatari ya kuwepo kwa uhaba wa chakula mwaka huu.

❹ Hii inamaanisha tatizo hili linakumba ulimwengu mzima wala si laana kwa mataifa ya Afrika kama wanavyodai baadhi yetu. Jamii yoyote ile inayokabiliwa na njaa huwa katika hatari kubwa ya kukumbwa na magonjwa mbalimbali.

❺ Kinga ya kwanza ya magonjwa katika mwili wa binadamu ni lishe nzuri. Kwa hivyo anayekosa chakula huwa rahisi kuugua ama kulemewa na ugonjwa. Wakati njaa na magonjwa yanapokabili binadamu, nguvu za kujitafutia riziki hukosekana. Matokeo yake ni umaskini ambao huathiri uchumi wa taifa kwa jumla.

❻ Masuala haya yote ya njaa, magonjwa, umaskini na uharibifu wa mazingira yanahusiana pakubwa na itakuwa vyema kuyatafakari kwa mapana zaidi. Wakati mwingi suala kuhusu uhifadhi wa mazingira linapozungumziwa watu huwaza tu kuhusu misitu.

❼ Lakini suala hilo linafaa kuchambuliwa zaidi na kuwekwa wazi kuwa mazingira yana uwezo wa kuathiri uhai wa binadamu kwa misingi tofauti. Kwa mfano, namna ya kushughulikia takataka ni suala la mazingira kwa sababu uchafu unaathiri moja kwa moja afya ya binadamu.

❽ Ni jukumu la kila mmoja wetu kuchukua hatua kulinda uhai wake kwa kudumisha mazingira bora. Sheria mwafaka pia zinahitajika kusaidia katika juhudi za kukabiliana na wanaochangia katika kuharibu mazingira.

Imetoholewa kutoka Valentine Obara, *Taifa Leo* (2014)

https://xtremepape.rs/

**Kifungu B**

# Warembo wa Miss Universe Tanzania 2014 waanza kambi



❶ Warembo wa Miss Universe Tanzania 2014 wameanza rasmi kambi katika hoteli yenye hadhi ya kipekee. Hii ni kwa ajili ya kujiandaa kwa fainali ya Miss Universe Tanzania 2014 itakayofanyika tarehe 2 mwezi Oktoba.

❷ Miss Universe Tanzania pia imeandaa mafunzo mbalimbali kwa ajili ya kuwapa warembo ili kujitambua kama vijana na kama wanawake. Mafunzo hayo yatakuwa yakitolewa na wataalamu mbalimbali kutoka katika nyanja tofauti.

❸ Mkurugenzi wa kampuni hii mashuhuri ambaye pia ndiye Mkurugenzi na Muandaaji mkuu wa Kitaifa wa mashindano haya Bi. Maria Sarungi Tsehai amesema usajili wa mwaka huu umefanyika katika mikoa mitano ya Tanzania na warembo zaidi ya 70 walisajiliwa kwa mashindano haya.

❹ Kambi ya Miss Universe Tanzania 2014 imekamilishwa na warembo 12 kutoka mikoa mitano ya Tanzania ambayo ni Arusha, Mwanza, Mbeya, Iringa na Dar es Salaam pamoja na mrembo mmoja kutoka Zanzibar. "Tumechagua warembo ambao wameonyesha uwezo wa kujitambua na kuelewa umuhimu wa kushiriki katika mashindano makubwa kama haya. Tuna wanafunzi wa vyuo wanaosomea udaktari, uhandisi, uhasibu na pia tuna akina dada wajasiriamali. Tunafurahi kuona kila mwaka warembo wetu wanazidi kujitambua na kazi yetu kubwa ni kuwaendeleza," alisema Sarungi.

❺ Pamoja na zawadi ya fedha taslimu, mshindi wa Miss Universe Tanzania 2014 atapata fursa ya kutangaza bidhaa mbalimbali na kufanya kazi za kijamii. Pia kama ilivyo ada kwa mwaka wa nne sasa, mshindi atapewa nafasi (*udhamini*) ya kusoma New York Film Academy, Marekani.

❻ Mashindano ya Miss Universe Tanzania yamedhaminiwa na makampuni kadha wa kadha mashuhuri. Makampuni haya yamewasaidia mno vijana ili kupata riziki yao ya kila siku. Kuna mifano mingi ya vijana kutoka jamii maskini ambao sasa wanajiweza kimaisha baada ya kusaidiwa.

Imetoholewa kutoka, www.fullshangweblog.com (2015)



https://xtremepape.rs/

**Kifungu C**

## Madereva wa mabasi ya wanafunzi kuweni makini

❶ Ndugu Mhariri,
Nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kueleza kero, yangu ambayo ninaamini si tu ni kero bali ni jambo la kufuatilia na linalostahili kuchukuliwa hatua mapema kabla halijaleta madhara kwa wahusika. Muda wa asubuhi nimekuwa nikishuhudia magari mengi ya kubeba wanafunzi wa shule mbalimbali kuanzia wale wa elimu ya awali (chekechea) hadi sekondari yakiwa barabarani katika harakati za kupakia wanafunzi kuwapeleka shuleni na hata muda wa jioni kuwarudisha nyumbani.

❷ Kinachosikitisha ni jinsi madereva wa magari haya wanavyoendesha pasipokuwa na makini wala kuwa na huruma. Magari haya yamekuwa yakiendeshwa kwa fujo bila kufuata taratibu za usalama barabarani.

❸ Wamekuwa wakipita magari mengine kwa mwendo wa kasi sana, kupita pembeni mwa barabara bila kujali kama kuna mitaro mikubwa au kuna wapita njia, jambo ambalo linahatarisha usalama wa watoto waliomo ndani ya mabasi hayo.

❹ Najiuliza hivi, madereva hawa huwa hawapewi mafunzo yoyote au muongozo wowote wanapokuwa barabarani ili kulinda usalama wa watoto wetu? Ni kwa nini basi wasijaribu kutafuta utaratibu wa kuwawezesha kuepuka foleni kwa usalama zaidi? Ni vyema madereva hawa watambue kuwa si tu wanawaendesha hawa wanafunzi kwa kuwa ni ajira yao, lakini wakumbuke wamebeba roho za watu ambao ni watoto wadogo wanaoandaliwa kwa ajili ya taifa la kesho.

❺ Ni vizuri **[ – X – ]** na taasisi zinazohusika zikaweka **[ – 27 – ]** na sheria **[ – 28 – ]** kwa madereva hawa ili kuepuka **[ – 29 – ]** ambazo zinaweza kuleta matatizo kwa watoto wasio na **[ – 30 – ]**. Tukumbuke kuwa "usipoziba ufa, utajenga ukuta".
Natumai kilio changu kitawafikia wahusika.
Ni mimi rafiki wa elimu.
Irene Mkinga

Imetoholewa kutoka *Rai* (2013)

https://xtremepape.rs/

**Kifungu D**

# Utalii ukiangamia uchumi matatani

❶ Kuongezeka kwa visa vya utovu wa usalama, ujangili dhidi ya wanyamapori na kutolewa kwa tahadhari za kuzuru Kenya ni baadhi ya mambo yanayoendelea kuathiri vibaya sekta ya utalii nchini.

❷ Licha ya matukio hayo yote, idara hiyo ilifufuka na ikashamiri baada ya hali kutulia na watalii kuendelea kuzuru Kenya. Baadhi ya mambo yanayoshuhudiwa kwa sasa si mageni kwa hivyo washikadau katika sekta ya utalii wanapaswa kuangazia mbinu za kuinua sekta hiyo tena badala ya kuendelea kushutumu mataifa ya magharibi kwa hatua waliyochukua.

❸ Ni bayana kuwa sekta ya utalii ina umuhimu mkubwa katika uchumi wa kitaifa na pia ni kigezo kikuu kuafikia Ruwaza ya 2030* kwa hivyo masuala ya yanayoiathiri yanapaswa kushughulikiwa kwa makini bila kuingizwa siasa na serikali pamoja na mrengo wa upinzani.

❹ Japo kuna uwezekano wa kuokoa sekta hii tena, twakwimu zinaonyesha kuwa inaendelea kudorora. Mnamo 2012 mapato ya sekta ya utalii yalishuka kwa asilimia kubwa. Mapato ya sekta hiyo yalikuwa chini jambo ambalo linadhihirisha kufifia kwa kiungo hiki muhimu cha uchumi wa Kenya.

❺ Kando na kushughulikia masuala ya usalama na ujangili nchini, serikali inapaswa kupunguza ushuru unaotozwa watalii wanaozuru maeneo mbalimbali nchini kama njia mojawapo ya kuwavutia watalii zaidi.

❻ Hatua ya Waziri kuteua kamati ya kuokoa sekta ya utalii ni ya kuungwa mkono lakini serikali inapaswa pia kupunguzia wageni gharama ya kutalii Kenya. Serikali inapaswa kuweka mikakati ya kuimarisha mandhari ya kukua kwa utalii nchini na kushirikiana na nchi za magharibi kukabiliana na visa vya utovu wa usalama nchini badala ya kuelekeza lawama mataifa hayo kwa kuzorota kwa sekta ya utalii.

❼ Kamati iliyoteuliwa inapaswa pia kulenga watalii wa kikanda bila kuangazia tu wageni wa Magharibi. Mpango wa kuanzisha visa vya pamoja katika mataifa ya Afrika Mashariki unapaswa kutiliwa nguvu ili kuhakikisha kuwa vizingiti vya raia wa mataifa jirani vimeondolewa ili kuhakikisha kuwa watalii wameendelea kuzuru Kenya.

❽ Mradi wa "Tembea Kenya" unaolenga kuwashawishi Wakenya kutembelea maeneo tofauti ya nchi pia ni wa kuungwa mkono. Serikali za Kaunti zinapaswa kuimarisha vivutio vya watalii vilivyo katika maeneo yao ili kutoa nafasi zaidi za utalii nchini.

Imetoholewa kutoka, Wycliffe Muia, *Taifa Leo* (2014)

* Mpangilio maalum wa jambo

https://xtremepape.rs/